**INTER ISLAMIC MOCK EXAMIMNATION**

**KISWAHILI 2**

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**

**2026**

1. Mtahiniwa anapaswa kueleza kwa ufupi mbinu za kifani zilizojitokeza katika shairi alilopewa.
   - **MUUNDO**
     Mtunzi ametumia muundo wa Tarbiya, yaani mistasri minuo kila beti kuanzia beti ya kwanza mpoaka ya mwisho.
   - MTINDO
     Mtunzi ametumia mtindo wa kimapokeo ule ufuatao urari wa vina na mizani. Mfano katika ubeti wa mwisho vina vya kati ni "ka" na vina vya mwisho ni "ya". Vilevile shairi hili limetumia mtindo wa usimulizi wa hadithi. Mfano katika ubeti wa kwanza mtunzi anasema "Kuna hadithi yak le, kwa babu nimepokeya".
   - WAHUSIKA
     Wahusika waliotumiwa na mtunzi wa shairi hili ni watu na wanyama.
   - MANDHARI
     Mandhari yaliyotumika na mtunzi wa shairi hili ni mandhari halisi kama vile shambani na porini. Mfano katika mshororo wa ubeti wa mwisho mtunzi anasema "akarudi porini, iliyoko kaumu"
   - MATUMIZI YA LUGHA
     - Lugha nyepesi
     - Matumizi ya lugha ya picha/taswira kimbwangai ikimaanisha ni nyani (viongozi wasaliti).
2. Mtahiniwa aeleze sifa za mtambaji kama ifuatavyo:
   Mtambaji ni mtu anayenena kazi ya fasihi. Mnenaji wa kazi za fasihi simulizi ni muhimu sana ili kufikisha ujumbe lengwa kwa jamii iliyokusudiwa. Kazi yake kubwa ni kuunganisha visa na matukio katika hadithi husika ili kuleta muunganiko wenye maana.
   SIFA ZA MTAMBAJI
   - Awe mbunifu ili aichangamshe hadhira
   - Awe na uwezo wa kuifahamu hadhira yake, Pamoja na mahitaji yao
   - Awe anaijua vyema utamaduni wa jamii husika
   - Awe anajua vyema lugha anayoitumia.

Shulelibrary.com

- Awe na mbinu za kifaraguzi
- Awe anakijua vyema kipera anachoshughulikia.
- Awe mcheshi ili aweze kuiteka hadhira yake
- Awe ni mjuzi wa mbinu za kisanaa, hususani utendaji
- Anapaswa kuelewa vema tabia za binadamu Pamoja na mikondo yao.

  **Alama 02 @ = 10**

3. Mtahiniwa afafanue kwa undani sababu za kufa na kufifia kwa sanaa za maonesho.

   Sanaa za maonesho – Ni sanaa zinazowasilishwa jukwaani sanaa hizi huwa na uga maalum wa kutendea, ambapo visa na matukio huwasilishwa hapo mbele ya watazamaji (hadhira).

   SABABU YA KUFIFIA

- Watu kutoelewa maana ya sanaa za maonyesho
- Watu kutothamini sanaa za maonyesho
- Kukosekana kwa uongozi bora wa kuendeleza gurudumu la sanaa za maonyesho
- Mipango na sera zinazosuasua kuhusu sanaa za maonyesho
- Uhaba wa maandishi yanayofaa kuhusu sanaa za maonyesho
- Uhaba wa fedha unaowakumba wasanii wa sanaa za maonyesho.

  **Alama 02 @ = 10**

4. Mtahiniwa afafanue kwa undani athari za udhamini katika kazi za fasihi

   - Udhamini ni hali ya mtu, watu au shirika Fulani kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia kitu Fulani, kuna aina mbili za udhamini, udhamini wa nguvu na udhamini wa ushawishi.

   **ATHARI ZA UDHAMINI**

   - Mtu aliyedhaminiwa huandika matakwa ya mdhamini tu.
   - Ufafanuzi wa kidata na maudhui lazima uendeane na mtazamo wa mdhamini.
   - Kazi za fasihi huwa ni mali ya mdhamini
   - Waandishi huanza kuandika kazi zao kwa kupenda pesa
   - Udhamini husababisha kuzuka kwa fasihi pendwa
   - Uandishi wa kikasuku

   **Alama 02 @ = 10**

Shulelibrary.com

5. Mtahiniwa aeleza vipengele vya mtindo vilivyojitokeza/vilivyotumiwa na wasanii wa ushairi.

Mtindo ni kipengele cha fani ambacho watunzi wa mashairi hukitumiwa kwa upana wake.

**VIPENGELE VYA MTINDO**

- Mtindo wa kisasa shairi la "Ngulu wapaona"
- Mtindo wa kidato shairi la "Udangoni", "Wasia"
- Mtindo wa kimapokeo shairi la "Fikira za waungwana"
- Mtindo wa masimulizi – shairi "Manzese mpaka Oysterbay"
- Mtindo wa swali – Manzese mpaka Oysterbay

**KIMBUNGA**

- Mtindo wa msisitizo mfano neno kujitawala 07 "Kujitawala".
- Mtindo wa swali/kuuliza swali shairi la "Mnapata kitu gani: .
- Mtindo wa **kimapokeo** katika shairi la "Kimbunga"

**Utangulizi = Alama 01**

**Kiini: Hoja 6 @ 3 = Alama 18**

**Hitimisho: Alama 01**

Shulelibrary.com

6. Mtahiniwa aeleze kwa kina namna wasanii walivyoakisi jamii zao kama ifuatavyo:

Mtahiniwa anatakiwa anoneshe msimamo wake kwa kubadili au kupinga kauli. Ni kweli wasanii hutumia sanaa zao kkuakisi yaiyomo katika jamii, kutokana na ukweli kuwa wasanii ni zao la jamii.

**CHUNGU TAMU**

- Suala la matabaka "Chatu na kuku"
- Suala la dhuluma "Chanz oni wenye kauli"
- Uongozi mbaya "Chini ya mti mkavu"
- Suala la mapenzi "Daktari Askari"

**FUNGATE YA UHURU**

- Uongozi mbaya "Viongozi wa Afrika"
- Kujitoa mhanga "Gorilla"
- Ukoloni mamboleo "Kunguru"

**Utangulizi = alama 02**

**Kiini: Hoja 8 @ 2 = alama 16**

**Hitimisho = Alama 02**

**JUMLA : Alama 20**

7. Mtahiniwa anapaswa kuonesha matumizi ya (Taswira) Jazanda katika tamthiliya alizosoma

**MORANI**

- Nguzo ya Uswezi – amali za asimio la Arusha
- Mizuka katika shamba la Tajiri – Tabaka la wanyonge
- Dongo – Wanamapinduzi
- Mti nje ya ofisi Pamoja na wachawi – Wahujumu Uchumi.
- Morani – vijana wanaotakiwa kuungana kuleta mabadiliko katika jamii.

**KIVULI KINAISHI**

- Kivuli kinaishi – Mawazo ya kimapinduzi yaliyokwisha pandikizwa kudai haki na usawa.
- Unga wa ndere – Itikadi zinazomfanya mtu katika tabaka tawala akubalike na kushika miiko.
- Giningi – ngazi ya utawala wa juu katika jamii.
- Unga wa rutuba – Elimu ya kujitambua katika jamii na kuelimisha wengine kuhusu haki zao.
- Mdundo wa ngoma – Kitendo cha kufuata amri za tabaka tawala.

**Utangulizi : Alama 02**

**Kiini: Hoja 8 @ alama 16**

**Hitimisho: Alama 02**

**JUMLA ALAMA 20**

Shulelibrary.com

8. Mtahiniwa anapaswa kueleza ni kwa namna gani tamaa imesababisha kuibuka kwa migogoro katika riwaya mbili alizosoma kati ya zifuatazo.

Tamaa ni hali au hamu ya kutaka au kutamani kupata au kutokea jambo Fulani. Hivyo basi hali hii baina ya wahusika ilipelekea kuibua migogoro ifuatayo:

**MFADHILI**

Nunu, Boaz na Bi Hanuna, hii ni kutokana na Boaz na Nunu walikuwa na tamaa ya kufahamu mahali alipo Gadibula, ikawalazimu kumteka Bi Hanuna ili awapeleke alipo mdogo wake.

- Mgogoro baina ya Nunu na Jerry hii ni kutokana na tamaa za Jerry kumsaliti rafiki yake Dania.
- Mgogoro kati ya Gadibullah na Dania, ulitokana na Dania kuwa na tamaa ya kuchukuliwa nafasi yake ya kazi na Gadibullah.
- Mgogoro baina ya Dania na Jerry, ulitokana na tamaa za Jerry Kwenda kimasomo nje ya nchi na kumuacha Dania akijiingiza kwenye ulevi uliokithiri.
- Mgogoro kati ya Gadibullah na Nyambuja, ni kutokana na tamaa za Nyambuja kutoka kimapenzi na rafiki wa Gadibullah.

**VUTA n'KUVUTE**

- Mgogoro baina ya Yasmini na wazazi wake, kutokana na tamaa za wazazi wake kumuozsha kwa Bwana Raza ambaye amemzidi umri.
- Mgogoro kati ya Bwana Raza na Yasmini, ni kwa sababu ya tamaa za Bwana Raza kumuoa binti mdogo aliyemzidi umri.
- Mgogoro kati ya wakoloni na Waafrika, ni kutokana na tamaa za wakoloni kutaka kuendelea kutawala Waafrika kiuchumi na kisiasa.
- Mgogoro kati ya Bukheti na Bwana Raza, kutokana na tamaa za Bukheti kumpenda mke wa Bwana Raza (Yasmini).
- Mgogoro baina ya Yasmini na nafsi yake, kutokana na Yasmini kumpenda kimapenzi Bukheti wakati yupo ndani ya ndoa na Bwana Raza.

**USIKU UTAKAPOKWISHA**

- Mgogoro kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa kwa tabaka tawala kuwa na tamaa ya kutaka
- Mgogoro kati yam gambo na walalahoi, kutokana na mgambo kuwa na tamaa ya kuchukuwa mali za walalahoi.

**KUFIKIRIKA**

- Mgogoro kati ya mjinga (Utubusara) na mwerevu kutokana na utabusara kutaka kumuelimisha mwenzake juu ya mambo mbalimbali katika jamii.
- Mgogoro wa kinafsi unamhusu mfalme, hii ni kutokana na kuwa na tamaa ya kutaka kumpata mtoto wa kurithi.
- Mgogoro baina ya Waziri Mkuu na wajumbe. Hii ni kutokana na tamaa za Waziri Mkuu kutaka kubadilisha sheria za nchi.

Shulelibrary.com

**Utangulizi : Alama 02**

**Kiini : Hoja 8 @ 2 = alama 16**

**Hitimisho : Alama 02**

**JUMLA ALAMA 20**

Shulelibrary.com